

Jina la Mwanafunzi

.....□□□□□□□□  
□□□□□□□□□□□□□□□□□□□□□□□□□□□□

**YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI HEMTOYE  
WILAYA YA LUSHOTO MKOA WA TANGA. MWAKA 2021**

**1.0. Utangulizi:**

Ninafurahi kukuarifu kwamba umechaguliwa kujiunga na kidato cha Kwanza Katika shule hii mwaka 2021 Shule ya Sekondari Hemtoye

Muhula wa kuanza masomo unaanza tarehe 11/1/2020. na mwisho wa kuripoti ni tarehe 19/1/2020 ndani siku saba.

**2.0 Mambo muhimu ya kuzingatia**

**2.1 Sare za Shule**

**WAVULANA**

- Sare ya shule hii ni Suruali mbili za rangi nyeusi kitambaa namba moja zisizobana
- Mashati mawili meupe ya mikono mifupi
- Soksi nyeusi jozi mbili na viatu vyeusi vya kufunga kwa kamba visiwe na kisigino kirefu
- Sweta rangi ya blue bahari

**WASICHANA**

- Sketi mbili za rangi nyekundu ndefu za heshima mshono rinda boksi
- Mashati meupe mawili ya mikono mifupi na hijabu nyeupe isiwe na urembo wowote na iwe usawa wa mabega
- Viatu vyeusi vyenye visigino vifupi vya kufungakamba
- Soksi jozi mbili nyeupe
- Sweta rangi blue bahari

**VIFAA VYA KUJIFUNZIA**

Mwanafunzi anatakiwa awe na vifaa vifuatavyo;Daftari kubwa (quare 3) 10,madaftari madogo ya msomi 10,kalamu za wino za kutosha,penseli za kutosha,dictionary ya English-English,

## **VIFAA VYA USAFI**

Ndoo ndogo, fagio la chelewa na panga.

### **3.0 Makosa Yafuatayo Yanaweza Kusababisha Kufukuzwa au Kusimamishwa shule.**

- a) Wizi.
- b) Uasherati na ushoga.
- c) Ubakaji.
- d) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji bangi, cocaine, mirungi, kubeli na kadhalika.
- e) Kupigana au kupiga.
- f) Kuharibu kwa makusudi mali ya umma.
- g) Kudharau Bendera ya Taifa.
- h) Kuwa mjamzito/kupata mimba.
- i) Kuoau au kuolewa.
- j) Kutoa mimba.
- k) Kugoma, kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu.
- l) Kukataa adhabu kwa makusudi.
- m) Kuwa na simu ya mkononi shuleni.

4.0 Mambo Mengine Muhimu yanayopaswa kukamilishwa na kuwasilishwa shuleni na mwanafunzi.

- a) Medical Examination Form, ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa hospitali ya Serikali. Fomu hii itakabidhiwa kwa Mkuu wa Shule mara utakaporipoti shuleni.
- b) Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi na mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai.
- c) Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule.

5.0 Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII  
MKUU WA SHULE**

*Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania*

**OR-Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa**

Shule ya Sekondai Hemtoye S.L. P 259 Lushoto.

**FOMU YA KUKUBALI NAFASI**

Ahadi ya Mzazi na Mwanafunzi kukiri na kukubali Sheria,Kanuni,Taratibu na Kutii Maagizo Halali ya shule.

**A. IJAZWE NA MWANAFUNZI MWENYEWWE**

1. Majina kamili\_\_\_\_\_
2. Tarehe ya kuzaliwa\_\_\_\_\_
3. Dhehebu\_\_\_\_\_
4. Mahali alipozaliwa\_\_\_\_\_Wilaya\_\_\_\_\_

Nimesoma maagizo yote ya kujiunga na Shule ya Sekondari □□□□□□□..  
na nimekubali kutimiza masharti na sheria zote za shule.

**SAINI YA MWANAFUNZI ..... TAREHE**□.....□□□□□□□

**B. IJAZWE NA MZAZI/MLEZI MWENYEWWE**

1. Majina kamili\_\_\_\_\_
2. Wewe ni Mzazi (**NDIYO/HAPANA**) Mlezi (**NDIYO/HAPANA**) kata isiyohusika.
3. Kazi yako ni\_\_\_\_\_
4. Anuani ya nyumbani/kazini/ yoyote ya karibu\_\_\_\_\_
5. Namba ya simu\_\_\_\_\_

Mimi Mzazi/Mlezi nimesoma maelezo yote na kuyaelewa vizuri. Nitakuwa tayari kutimiza wajibu wangu kama Mzazi/Mlezi wa mwanafunzi, ikiwa ni pamoja na kufuatilia maendeleo ya mwanafunzi Shuleni na nyumbani. Pia nipo tayari kumlipia mwanangu chakula cha mchana awapo shuleni. Niko tayari kuchukuliwa hatua za kisheria pale mwanangu atakapotoroka shule au kuacha shule pasipo kumfuatilia.

**SAINI YA MZAZI/MLEZI**□..... **TAREHE**□□.....□□



I certify that the above mentioned pupil is fit/unfit to pursue Secondary Studies.

Name of Officer.....

Signature.....

Date.....

Officer Stamp